



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
WIZARA YA AFYA

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**

Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)



**TANGAZO**

**KUFUNGULIWA KWA DIRISHA LA MAOMBI YA USAJILI KWA NJIA YA  
MTANDAO**


Baraza la Wataalam wa Maabara linachukua nafasi hii kuwajulisha Wataalam wote wanaotarajia kufanya maombi ya usajili wa awali (Provisional Registration), Usajili wa Enrollment (ERP) na usajili wa kudumu (FRP) kuwa dirisha la usajili kwa njia ya mtandao (online Registration System) limefunguliwa leo tarehe **20 Aprili 2022** na litafungwa tarehe **06 Juni 2022**.

Maombi yote ya usajili yatafanyika kwa njia ya mtandao kupitia anwani hii [hprs.moh.go.tz](http://hprs.moh.go.tz).

Aidha, Baraza linasisitiza kwa Wataalam waliofanya mitihani ya Baraza kwa mwezi Machi na Aprili 2022 wasiingie kwenye mfumo mpaka pale watakapopata matokeo yao ya mitihani na watakapopewa taarifa za kuingia kwenye mfumo kutoka ofisi ya Msajili.

Muongozo wa namna ya kujisajili kwenye mfumo (Health Practitioners Registration System Manual) unapatikana kwenye tovuti ya Baraza ([www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)). Kwa msaada Zaidi piga simu za ofisi 0734005777.

Upatapo tangazo hili mtaarifu na mwenzako.



Imetolewa na

Msajili  
Baraza la Wataalam wa Maabara.